S. KITUO CHA MATATIZO YA UBAKAJI HUFANYA NINI?

J. Kituo cha Matatizo ya Ubakaji ni kikundi cha wanawake. Tunatoa msaada kwa wanawake wengine ambao wamekuwa na masaibu mabaya katika nchi yao au nchini Uingereza. Masaibu haya yanawezakuwa yametekelezwa na askari, polisi au majeshi, magaidi, na wageni katika mtaa au mtu ambaye mwanamke anamjua vizuri sana- hata mume wake.

Tunaamini kwamba hakuna yeyote ana haki ya kumuumiza mwanamke au mtoto kwa njia yoyote ile au kumfanya afanye mambo ambayo yanamkasirisha au kumwaibisha.

Ikiwa umekuwa na masaibu ambayo yalikufanya ujihisi vibaya, yalikuumiza au kukuaibisha, unaweza kuzungumza nasi kuyahusu. Kuna wanawake hapa ambao watakusikiliza na kukusaidia, lakini hawatakuhukumu kwa sababu ya kile kilichofanyika.

Wafanyikazi wote wa Kituo cha Matatizo ya Ubakaji ni wanawake na ikiwa unahitaji mkalimani, tutahakikisha kwamba mkalimani pia ni mwanamke. Haustahili kulipia huduma yetu.

S. JAMBO FULANI LILINIFANYIKIA ZAMANI. BADO NINAPATA KUMBUKUMBU AMBAZO ZINANIKASIRISHA NA KUNISHTUA. NINAWEZA KUPATA MSAADA KUTOKA KWA KITUO CHA MATATIZO YA UBAKAJI?

J. Ikiwa kuna jambo lililokufanyikia ulipokuwa mtoto ambalo lilikufanya ujihisi umeumia, umekasirika na kuaibika, unaweza kuzungumza nasi. Inawezakuwa haujazungumza na mtu mwingine mbeleni. Kitu fulani kinawezakuwa kimeileta kwa akili yako na sasa unahitaji kuizungumzia. Tunaweza kukusaidia na hatutakuhukumu kwa sababu ya kilichofanyika.

S. NI AINA GANI YA WANAWAKE WANAOFANYA KAZI KATIKA KITUO CHA MATATIZO YA UBAKAJI?

J. Wanawake wanaofanya kazi katika Kituo cha Matatizo ya Ubakaji ni wanawake wa kawaida kutoka jamii tofauti na tamaduni tofauti. Wafanyikazi wote wamefunzwa vizuri na wanaheshimiana na wanawake wanaotumia huduma yetu.

S. NILIBAKWA NA MWANAUME KATIKA JAMII YANGU NA ANASEMA KWAMBA ATAELEZEA KILA MTU MIMI NI MWANAMKE WA AINA GANI. NINAOGOPA NITAADHIBIWA.

J. Wanawake wengi, kutoka jamii zote, hutuambia kwamba walibakwa na wanaume wanaowajua. Mara kwa mara hao huogopa ya kwamba kila mtu atajua kuhusu jambo hili na kwamba wataaibika hadharani. Unaweza kuzungumza nasi kuhusu jambo hili na tutakuunga mkono.

S. NILIBAKWA NA ASKARI KATIKA NCHI YANGU YA NYUMBANI. NINAWEZA KUFANYA NINI?

J. Unaweza usifanye kitu chochote ili kuwashtaki wanaume hao waliokubaka, lakini unaweza kuwaambia mawakili ambao wanashughulikia dai lako la uhamisho kwamba jambo hili lilifanyika. Wafanyikazi wetu wanaweza kukusaidia na jambo hili.

S. BINTI YANGU PIA ALIBAKWA, LAKINI BADO YUKO UMRI WA MIAKA 14. NI WAPI NINAWEZA KUPATA MSAADA?

J. Katika Kituo cha Matatizo ya Ubakaji tunaweza kuwasaidia wanawake wachanga ambao wamezidisha umri wa miaka 13, ambao wamekuwa na masaibu mabaya katika nchi hii, na wanaume katika nchi yao au wakisafiri Uingereza.

S. MUME WANGU HUNIFANYA NIFANYE MAMBO AMBAYO YANANITISHA NA KUNIUMIZA. NINAWEZA KUFANYA NINI?

J. Mume wako hana haki ya kukutisha, kukuumiza au kukufanya ufanye jambo lolote ambalo hutaki kufanya. Mtu yeyote katika familia yako,au familia yake akikuumiza au kukufanya ufanye jambo lolote ambalo linakuaibisha, au kukufanya ujihisi vibaya, unaweza kuwasiliana nasi na tutajaribu kukusaidia.

S. SIKO KATIKA NCHI HII KIHALALI. MNAWEZA KUNISAIDIA?

J. Hata kama hauko katika nchi hii kihalali, una haki ya kuwa salama na kulindwa dhidi ya madhara. Ikiwa umeingizwa kimagendo nchini Uingereza kwa ajili ya ukahaba tunaweza kukuunganisha na mradi mwingine wa wanawake, ambao utakusaidia kupata usalama. Ikiwa unataka kwenda nyumbani, tunaweza pia kukuunganisha na mtu ambaye anaweza kukusaidia.

S. NINGEPENDA KUZUNGUMZA NA MTU KATIKA KITUO CHA MATATIZO YA UBAKAJI LAKINI SITAKI KUFANYA HIVYO MBELE YA WATOTO WANGU.

J. Hatuna mtu yeyote wa kuwaangalia watoto katika Kituo cha Matatizo ya Ubakaji lakini kama unataka kupata mtu wa kumwangalia mtoto, tunaweza kumlipa mtu huyo ili amwangalie mtoto wako au watoto wakati uko katika Kituo chetu. Hatuwezi kumlipa mume au mwenzi wako ili kuhudumia watoto wako, lakini unaweza kuomba rafiki au jirani kufanya hivi.

S. SIWEZI KUZUNGUMZA KIINGEREZA. NITAWEZA KUONGEA NA MTU ANAYEZUNGUMZA KISWAHILI?

J. Tunaelewa kwamba ni vigumu sana wakati huwezi kuzungumza na mtu moja kwa moja kwa sababu huwezi kuzungumza lugha hiyo, kwa hivyo sisi hutumia mkalimani kwa vikao vyetu. Daima sisi huhakikisha kwamba mkalimani ni mwanamke. Hata kama mwenzi au mume wako anataka kukutafsiria, hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu tunawatumia wakalimani waliyofunzwa tu. Wakalimani pia wanaelewa kuhusu kuhakikisha kitu chochote kinachojadiliwa kati yako na mfanyikazi wako wa msaada hakishirikiwi nje ya chumba cha msaada.

S. NIMEBAKWA NA NINAOGOPA KUWAAMBIA POLISI.

J. Sio lazima uzungume na polisi ikiwa hutaki.

Ikiwa umebakwa Glasgow kati ya siku 7 zilizopita unaweza kupiga simu mahali panapoitwa Archway ambapo unaweza kumwona daktari mwanamke na muuguzi mwanamke. Huko Archway unaweza kupimwa ikiwa utataka kubadili nia yako na kuwaeleza polisi baadaye. Mtu ambaye ni mnenaji wa Kiingereza atawapigia simu ili kuweka miadi.

Huko Archway unaweza pia kuwaona wafanyikazi wa msaada au washauri ambao pia ni wanawake na ambao watakusikiliza ikiwa unataka kuzungumza kuhusu kilichofanyika. Ikiwa huwezi kuzungumza Kiingereza, daktari wa Archway atahakikisha umepata mkalimani. Hakuna mmoja wa wanawake hawa atakayekuhukumu kwa sababu ya kile kilichofanyika na daima watakushughulikia kwa heshima.

Huko Archway unaweza kupanga upimwe magonjwa ya zinaa na HIV.

S. KWA HIVYO NINAWEZAJE KUWASILIANA NA KITUO CHA MATATIZO YA UBAKAJI?

J. Mawasiliano ya kwanza na Kituo cha Matatizo ya Ubakaji lazima yawe kwa Kiingereza lakini unaweza kuweka miadi nasi kupitia rafiki unayemwamini, mfanyikazi mkuu au mfanyikazi wako wa afya au daktari.

Tutahitaji kujua ni lugha gani unayopendelea kuzungumza au kutumia ili tuweze kuhakikisha tuna mkalimani mwanamke kwa miadi yako ya kwanza.

Unaweza kumleta mtu kwa miadi yako ya kwanza na sisi. Tuna mahali pazuri wanaweza kusubiri na kunywa chai au kinywaji baridi. Ikiwa utahitaji huduma ya watoto na usafiri wako kulipwa, mtu anayeweka miadi anapaswa kutujulisha ili tuweze kuhakikisha pesa ziko tayari unapokuja.